THE SALVATION ARMY INTERNATIONAL HEADQUARTERS

# Ujumbe wa Jenerali wa Krismasi ya Mwaka 2024

Nilipata nafasi mapema mwaka huu kuhudhuria Kongresi ya *Ushuhuda* ya Jeshi la Wokovu Teritori ya Magharibi Marekani. Yalikuwepo mambo muhimu mengi mwisho wa juma lile, lakini lile lililojitokeza zaidi kwangu lilikuwa zile hadithi za ajabu za mabadiliko. Wanaume na wanawake ambao maisha yao yalikuwa yamebadilishwa kwa sehemu kubwa walipokutana na upendo wa Mungu kwao katika Yesu Kristo. 'Kwa maana jinsi hii Mungu anaupenda ulimwengu…' – ndiyo, nimebadilisha wakati. Kwa kweli kifungu kinasomeka, 'Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe pekee' (Yohana 3:16). Na bado upendo wa Mungu ni halisi, wa kweli na wenye kina leo kama ulivyokuwa katika Siku ile ya Krismasi ya kwanza. Huu umebakia kuwa ushahidi mkubwa wa upendo wa Mungu na mpango wake kwa watu wote – zawadi ya Mwanawe, zawadi ya wokovu – sio tu wakati uliopita, bali kwa wakati uliopo vile vile. Hii ndiyo habari njema tunayoisherehekea wakati wa Krismasi.

Habari hiyo ilitabiriwa na nabii Isaya zamani: 'Maana kwa ajili yetu mtoto amezaliwa, tumepewa mtoto mwanamume; na uwezo wa kifalme utakuwa begani mwake; naye ataitwa jina lake, Mshauri wa Ajabu, Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele, Mfalme wa Amani. Maongeo ya enzi yake na amani hayatakuwa na mwisho kamwe' (Isaya 9:6-7).

Ilitangazwa tena na malaika Yesu alipozaliwa: 'Na katika nchi ile walikuwako wachungaji wakikaa makondeni na kulinda kundi lao kwa zamu usiku. Malaika wa Bwana akawatokea ghafla, utukufu wa Bwana ukawang'aria pande zote,wakaingiwa na hofu kuu. Malaika akawaambia, "msiogope, kwa kuwa mimi ninawaletea habari njema ya furaha kuu itakayokuwa kwa watu wote, maana leo katika mji wa Daudi amezaliwa, kwa ajili yenu, Mwokozi, ndiye Kristo Bwana. Na hii ndiyo ishara kwenu, mtamkuta mtoto mchanga amevikwa nguo za kitoto, amelazwa katika hori ya kulia ng'ombe." Mara walikuwapo pamoja na huyo malaika, wingi wa Jeshi la mbinguni, wakimsifu Mungu, na kusema, "Atukuzwe Mungu juu mbinguni, na duniani iwe amani kwa watu aliowaridhia" (Luka 2:8-14).

Biblia inatuambia wachungaji mara moja walikwenda alikokuwa Yesu, na baada ya kumwona mara moja walianza kusambaza habari. Napenda hilo! Walianza kuwashirikisha wengine waliyoyaona bila kuchelewa. Wachungaji walimtambua Yesu jinsi alivyokuwa – Mwokozi wao – na hawakupoteza muda kwenda nje na kutangaza habari njema. Ushuhuda wa namna gani!

Waamini toka wakati huo wameendeleza huduma ya kueneza neno la Mungu linalookoa, linalosamehe, kazi inayokomboa kupitia kwa Mwanawe, Mwokozi wetu, Yesu Kristo. Niliona na kusikia ushuhuda wa hili wakati wa *Ushuhudia* – watu wakiwashirikisha wengine habari njema ya nguvu ya Mungu ibadilishayo ndani na kupitia kwa maisha yao, vile vile kama wachungaji walivyofanya usiku ule zamani sana.

Katika kitabu hiki, 'Hatari Takatifu', Jenerali Shaw Clifton (Aliyestaafu) ameandika:'Krismasi imehitimishwa katika Yesu. Jina lenyewe Yesu linatosha katika historia yote kutangaza kwamba kuna Mwokozi. Kwa hiyo linafuata kimantiki kwamba kama kuna Mwokozi ni kwa sababu tunahitaji kuokolewa. Hata hivyo, kabla hatujatambua hitaji letu Mwokozi yupo. Ni yeye anayetuonyesha mahitaji yetu ya ndani, kwa upole akituhimiza kwa Roho wake Mtakatifu tuitikie mwaliko wake wa wokovu. Kwa hiyo Krismasi ni kugundua au kugundua tena au kumthibitisha tena Yesu kama Mwokozi, na katika kumgundua tunajigundua wenyewe na hali zetu halisi.'

Mungu bado anaweza kubadilisha mioyo ya wanaume na wanawake na kuwafanya waishi tena. Na kama wachungaji, tunaweza kushuhudia kwa waliotuzunguka kuhusu habari njema.

Krismasi hii, tunaposherehekea kuzaliwa kwa Mwokozi, hebu tumwombe Mungu atuwezeshe kwa nguvu za Roho Mtakatifu tueneze habari kuhusu Yesu, ili bado wengi zaidi waje wakutane na upendo wa Mungu kama ulivyofunuliwa katika zawadi ya thamani ya Mwanawe na Mwokozi wetu, Yesu, Mwana wa Mungu.

Kamishena Bronwyn anaungana nami katika kuomba baraka za Mungu ziwe juu yako majira haya ya Krismasi.

Lyndon Buckingham
Jenerali